## Maswali

1. Yusufu alifanya nini kwa hizo miaka 7 ya mavuno mazuri?
2. Nani alikuja Misri kununua nafaka?
3. Mbona Yusufu hakutambuliwa na ndugu zake?
4. Ndugu walifanya nini kilichotimiza ndoto za Yusufu kuwa kweli?
5. Yusufu aliambia nduguze nini?
6. Yusufu aliwambia lazima wakuje na nani ikiwa watakuja kununua chakula tena?
7. Yusufu aliambia nduguze nini walipokuja na Benyamini kununua chakula?
8. Yusufu aliambia nduguze kufanya nini?
9. Yakobo na familia yake waliishi wapi katika nchi ya Misri?
10. Mungu aliambia Yakobo nini?

## Majibu

1. Yusufu aliweka chakula kingi wakati wa hizo miaka 7 ya mavuno mazuri.
2. Ndugu wa Yusufu walikuja kununua nafaka.
3. Yusufu alikuwa mtawala wa Misri.
4. Ndugu zake waliinamia Yusufu.
5. Yusufu alisema kwamba walikuwa wapelelezi.
6. Yusufu aliwambia kwamba lazima Benyamini aje nao.
7. Yusufu aliwambia kwamba yeye ndiye ndugu wao Yusufu.
8. Yusufu aliwambia wawalete Yakobo na familia yao yote Misri.
9. Yakobo na familia yake walikaa Misri kwa eneo ya Gosheni.
10. Mungu alimwambia Yakobo kwamba familia yake itakua na iwe taifa kubwa kule Misri. Mungu atakuja tena kuwarudisha wazao wake Isreali katika nchi yao.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 1 Mwaka wa 3

# 11 Familia ya Yusufu inakuja Misri

## Marejeo

Mwanzo 41:53–57; 42:1–20; 43:1–7;
Mwanzo 45:1–10 na 21–28; 46: 1–4

## Kiini cha somo

Kuonyesha tabia muhimu nzuri za Yusufu za kuwasamehe ndugu zake. Mungu hushulikia maisha ya watu wanaomwamini na ana mpango nao.

## Maneno maalum

11.1 Yusufu mtawala + kuuzwa tena + Yakobo + ndugu + Misri + sio Benyamini.
11.2 Yusufu mtawala + ndugu + hakutambulikana + inama chini + wapelelezi + gereza + leta ndugu
11.3 Simeoni + gereza + nyumbani + Yakobo + Misri + Benyamini
11.4 Yusufu + ndugu + furaha + samehe + leta Yakobo
11.5 Mkokoteni ya chakula + Yakobo + Yusufu yu hai + Misri + Gosheni + Mungu + taifa kubwa + wazao wanarudi Isreali

**11.1** Farao alifanya Yusufu kuwa mtawala wa nchi ya Misri. Kwa muda wa miaka saba ya mavuno nyingi, Yusufu aliweka chakula kingi kwa maghala ya miji. Ilipotimia wakati wa njaa, Yusufu alifungua hizo maghala za nafaka na kuwauzia Wamisri.

Hakukuwa na chakula kwa nchi zingine. Watu walikuja Misri kununua chakula. Yusufu alikuwa ameweka chakula kingi kwa hivyo aliuzia watu wote. Babake Yusufu na nduguze hawakukuwa na chakula. Yakobo aliposikia kwamba kuna chakula Misri, aliambia wana wake, "Enendeni Misri, mnunue chakula ili tuishi lakini tusife."

Ndugu wa Yusufu waliondoka kwenda inchi ya Misri. Lakini Yakobo hakutaka waende na Benyamini, mwanawe mdogo. Alisema, "Sitaachilia Benyamini aende kwa maana kunaweza kutokea ajali. Sitaki kumpoteza Benyamini vile nilimpoteza Yusufu aliporaruliwa kwa vipande vipande na wanyama wakali."

**11.2** Wale wandugu walisafiri kwenda Misri. Hawakujua kwamba ndugu wao Yusufu ndiye alikuwa mtawala kule. Yusufu aliwajua lakini wao hawakumtambua. Yusufu alikuwa amevaa kama Mmisri. Alizungumza lugha ya Wamisri. Alikuwa mtawala mkuu wa Misri.

Wandugu wake walimwinaia na kuuliza kama kuna nafaka ya kununua. (Unakumbuka ndoto za Yusufu kwamba ndugu zake watamwinamia? Wakati huu ndio hizo ndoto zilitimizwa.)

Yusufu alijifanya kwamba hawajui ndugu zake. Aliwauliza, "Mlitoka wapi?" " Sisi tulitoka Kanaani na tulikuja kununua chakula." Walimjibu Yusufu. Yusufu alijifanya kwamba hawajui. Aliwambia, "Nyinyi ni wapelelezi. Mmekuja kupeleleza nchi yetu."

Wandugu walimjibu, "La. Sisi tumekuja kununua chakula. Tulikuwa wandugu kumi na wawili. Mdogo ako na baba yetu nyumbani na mwingine alikufa." Yusufu alipaza sauti na kusema, "Nyinyi ni wapelelezi! Enda mlete ndugu wenu mdogo ndio nijue mnasema ukweli. Nitaweka mmoja wenu gerezani halafu wengine muende. Sitataka kumwona tena mpaka mtakapokuja na ndugu wenu mdogo."

**11.3** Simeoni aliachwa Misri gerezani. Ndugu wengine walipewa nafaka. Halafu wakaenda nyumbani kwa Yakobo, baba yao. Waliambia Yakobo yote yaliyofanyika Misri.

Walipokuwa wamekula chakula chote, Yakobo aliwambia waende Misri kununua chakula kingine na bure wangekufa. Yakobo aliachilia Benyamini aende nao vile Yusufu alikuwa ameamrisha.

**11.4** Yusufu alipoona ndugu zake alilia kwa furaha ya kuwaona tena. Aliwambia, "Mimi ni ndugu wenu mwenye mliuza Misri. Msiogope. Mungu alinituma hapa ili niokoe watu kutoka kwa njaa." Hao wandugu waliogopa walipojua kwamba huyu mtawala mkuu ni ndugu yao Yusufu. Walimuuza awe mtumwa. Lakini Yusufu aliwasamehe.

Yusufu alijua kwamba kuna miaka mingine mitano inakuja ya njaa. Alitaka kuhakikisha kwamba baba yake na familia wana chakula cha kutosha kwa miaka yote ya njaa. Yusufu aliambia ndugu zake, "Harakisha murudi kwa baba yangu. Mmwambie kwamba mimi ni hai na Mungu amenifanya kuwa mtawala wa nchi yote ya Misri." Yusufu alimbusu nduguye Benyamini. Aliwambia waende wamlete baba yake na familia zao zote.

**11.5** Yusufu aliwapa magari iliyojaa chakula wapelekee baba yake Yakobo. Walienda haraka kumchukua baba yao. Yakobo hakuamini kwamba mwanawe Yusufu alikuwa hai na ndiye mtawala wa nchi ya Misri. Lakini alipoona magari yamejaa chakula aliawaamini.

Alisema, "Mwanangu Yusufu yu hai? Nitaenda nimuone kabla nife." Yakobo na familia yake walifunga vitu vyao vyote na wakaenda kuishi Misri. Walienda kuishi Gosheni, ndio eneo nzuri sana kwa nchi ya Misri.

Mungu alikuwa ameambia Yakobo kwamba atafanya familia yake kuwa kubwa katika nchi ya Misri. Mungu atakuwa na Yakobo kwa hiyo nchi ya Misri. Baada ya miaka mingi, Mungu atarudisha uzao wake kwa nchi yao ya Israeli (Kanaani).